Josiah Hall
March 4, 2007

Mji wa Eldoret

Katika nchi ya Kenya kuna mji mdogo unaoitwa Eldoret. Eldoret ni mji mdogo lakini unakua. Una vivutio vingi hasa kwa sababu uko mbali sana kutoka kwa usawa wa bahari. Nitaandika kuhusu historia, jiografia, na vivutio vya Eldoret.

Historia ya Eldoret

Zamani, makabila mengi yalikaa katika mahali ambapo panaitwa Eldoret sasa. Kwanza kulikuwa na watu waliojenga nyumba ya mawe. Watu hawa waliitwa Sirikwa na walikaa katika Eldoret takriban mwanzo wa karne ya kumi na tisa. Lakini walikuwa na vita pamoja na Maasai na walishindwa. Halafu walihamia mlima wa Elgon. Kama ukienda mji wa Eldoret sasa unaweza kuona mabaki ya nyumba zao ambazo zinaitwa “Mashimo ya Sirikwa.” Baada ya vita Maasai walikaa Eldoret na baada ya kutoka makabila mengine yalifika, kwa mfano Kabila la Nandi na Kabila la Kalenjin. Lakini, ingawa kuna watu waliokaa mahali pa Eldoret hakukuwapo na mji wo wote. Ghafula watu wa nchi nyingine walifika.

Mwaka wa Elfu Moja Mia Tisa na Nane, watu kutoka Afrika Kusini walifika kwanza. Halafu watu kutoka Ulaya na Asia walifika pia. Watu hawa walikuwa wakulima na wafanyabiashara kwa hivyo walijenja majengo na kuanzisha mashamba. Mwaka wa wa Elfu Moja Mia Tisa na Kumi watu walijenga Posta katika shamba la Willy van Aardt. Shamba lilo liliitwa “Shamba Sitini na Nne” kwa sababu lilikuwako maili sitini na nne kutoka barabara ya gari la moshi ambayo ilienda Uganda kutoka Kibigori, kwa hivyo mji uliitwa “Sitini na Nne” pia. Sasa shamba hilo haliko. Baada ya miaka miwili Liwali aliamua kwamba alitaka kujenja majengo ya serikali katika “Sitini na Nne” halafu mahali pale palipewa jina jipya la Eldoret.

Wakati wa miaka ambayo ilifuata mji wa Eldoret uliendela kukua. Watu wengi walienda mji huo na mwaka wa Elfu Moja Mia Tisa Ishirini na Nne njia ya gari la moshi ilifika. Njia ya gari la moshi hiyo ni kutoka mji wa Kibigori na inaendelea mpaka nchi ya Uganda. Halafu mwaka wa Elfu Moja Mia Tisa Ishirini na Nane mji wa Eldoret ulianza kupata maji kutoka mto wa Sosiani. Pia mwaka wa Elfu Moja Mia Tisa Thelathini na Tatu Kampuni ya Umeme ya Afrika Mashariki ilijenja kituo cha umeme katika mji wa Eldoret.

Jiografia ya Eldoret

Eldoret ni mji mmoja wa Kenya Magharibi. Uko mashariki ya Ziwa la Victoria na kaskazini magharibi ya jiji la Nairobi. Pia Eldoret iko kusini ya milima midogo ya Cherangani. Eldoret ni baina ya futi elfu saba mpaka elfu tisa juu ya usawa wa bahari. Kwa sababu ya mwinuko huo wanaokimbia wengi hufanya mazoezi yao katika Eldoret. Mji wa Eldoret uko jimbo la Bonde Kuu, wilaya ya Uasin Gishu. Mto wa Sosiani uko karibu sana na Eldoret.

Katika mwaka wa elfu moja mia tisa kumi na mbili barabara ya gari la moshi ile ilifika katika mji wa Eldoret. Baada ya barabara ya gari la moshi kufika watu wengi walikuja mjini Eldoret. Sasa Eldoret ni mji mkubwa wa tano wa nchi ya Kenya. Maji kwa mji wa Eldoret yanatoka mto wa Sosiani. Watu wanaokaa mjini wanatumia maji yale. Pia kuna mashamba mengi ambayo yanazunguka mji wa Eldoret. Lakini katika Eldoret kuna viwanda vingi pia.

Vivutio

Eldoret ni mji wa watu wengi maarufu. Kwa mfano Daniel Toroitich arap Moi ambaye alikuwa Rais wa Kenya, Kipchoge Keino, na kadhalika. Daniel Moi alizaliwa mji wa Sacho, wilaya ya Baringo. Lakini alienda shule kuwa mwalimu katika Kapsabet, karibu na mji wa Eldoret. Moi ni mtu wa kabila la Kalenjin ambalo linakaa karibu na mjini Eldoret. Badala ya kufundisha Moi aliamua kujaribu kuingia kwa serikali. Kabla ya Kenya kupata Uhuru Moi

alikuwa waziri wa Elimu. Baada ya Kenya kupata Uhuru Moi alichaguliwa na Rais wa Kenya aliyeitwa Jomo Kenyatta kuwa Kaimu wa Rais. Kenyatta alikufa mwezi wa tisa tarehe ishirini na mbili, mwaka elfu moja mia tisa sabini na nane na baada ya hapo Moi alikuwa Rais wa Kenya. Alikuwa Rais mpaka mwaka elfu mbili na mbili. Watu wengi, hasa watu wa kawaida, walipenda Moi mwanzoni mwa utawala wake. Lakini mwishoni mwa utawala wake watu wengi waliamini kwamba Moi alikuwa fisadi sana, kwa hivyo walitaka rais mpya. Majeno mengi na pia shule nyingi ziliitwa Moi. Shule moja kutoka hizi ni Chuo Kikuu cha Moi ambacho kiko Eldoret.

Kuna vyuo vikuu saba nchini Kenya. Chuo Kikuu cha Moi kilianzishwa na Bunge katika mwaka elfu moja mia tisa themanini na nne. Sasa wanafunzi wengi, takriban elfu kumi na nne mia nane hamsini na tano (katika mwaka elfu mbili na sita) wanasoma katika Chuo Kikuu cha Moi. Ni shule nzuri na kina vitivo kumi na vitatu. Pia Chuo Kikuu hiki kina mabewa manne. Kuna bewa kuu, Mjini, Chepkoilel, Kitale, na Nairobi. Kila mabewa yana majengo ya kuhusu elimu, mabweni, na uwanja wa michezo.

Kuna vivutio vingine katika mji wa Eldoret. Kivutio kikubwa kimoja ni Uwanja wa Ndege wa Kimatafia wa Eldoret. Si Uwanja wa Ndege mkubwa lakini ni mzuri sana. Uwanja wa Ndege huu ulijengwa mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na tano. Kwa mfano, mwaka wa Elfu Mbili na Moja watu walisema kwamba Uwanja wa Ndege huu ulikuwa safi kuliko mwingine wo wote. Una njia moja kwa ndege kutoka na kufika moja. Njia hii ni barabara ya lami na ina urefu wa kilomita tatu nukta tano. Kwa kawaida ndege ambazo zinafika Uwanja wa Ndege wa Eldoret zinaleta mifugo na vitu vya biashara, lakini wakati mwingine ndege zinafika zinazoleta watu.

Pia kuna viwanda vingi mjini Eldoret. Kuna wakulima wengi karibu na Eldoret. Kwa hivyo wakulima wale huleta mavuno yao viwandani. Huleta mavuno kama ngano na mahindi.

Viwanda vingine ni kama kiwanda cha kusokota. Pia wakulima wa Eldoret wanatengeneza jibini bora zaidi.

Mji wa Eldoret una sifa njema kwa sababu ni juu kutoka usawa wa bahari sana kwa sababu mji uko milimani. Kama unataka kuwa mkimbiaji mzuri sana ni lazima kufanya mazoezi mengi. Kama ukifanya mazoezi yako katika mahali ambapo pako juu sana kutoka usawa wa bahari utaweza kukimbia upesi zaidi na kwa wakati mrefu zaidi. Kwa hivyo wakimbiaji wa Kenya wengi wanaenda mjini Eldoret kufanya mazoezi yao. Mfano mmoja wa mkimbiaji ambaye alifanya mazoezi karibu na mjini Eldoret ni Kipchoge Keino.

Kipchoge Keino alizaliwa mwaka wa elfu moja mia tisa na arobaini, mjini Kipsamo, wilaya ya Nandi. Alikuwa mkimbiaji mzuri sana sana. Alianza kukimbia katika mwaka wa elfu moja mia tisa sitini na mbili katika Mashindano ya Jumuiya ya Madola mjini Perch nchini Australia. Baadaye alienda Mashindano ya Dunia mwaka wa elfu moja mia tisa sitini na nne. Kila mashindano aliendelea kusitawi. Alivunja rekodi ya dunia katika shindano la mbio la mita elfu tatu na la mita elfu tano. Halafu alienda jiji la Mexico City kwa Mashindano ya Dunia ya mwaka wa elfu moja mia tisa sitini na nane. Alishinda kabisa na alipata kuwa wa kwanza katika shindano la mbio la mita elfu moja na mia tano (alipata medali ya dhahabu), na alikuwa wa pili katika shindano la mbio la mita elfu tano (alipata medali ya fedha). Alienda Mashindano ya Dunia ya mwaka wa elfu moja mia tisa sabini na mbili pia. Mashinando ya Dunia yale yalikuwako jijini Munich nchini Ujerumani. Alishinda katika shindano la farasi kwenda moja kwa moja la mita elfu tatu. Pia alikuwa wa pili katika shindano la mbio la mita elfu moja na mia tano. Kipchoge Keino alifanya vitu vingine tofauti na kukimbia. Alifanya vitu vya huruma na sasa anasaidia wakiwa.

Kivutio kingine cha mji wa Eldoret ni hoteli. Kuna hoteli nzuri mjini Eldoret. Kwa mfano kuna hoteli ya Sirikwa. Hoteli hii ni kilomita ishirini kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Eldoret. Ni hoteli ya nyota tatu kwa hivyo ni hoteli nzuri tu. Bei ni dola sitini na tano kwa usiku mmoja (katika shilingi ni takriban elfu nne mia tano na ishirini). Hoteli nyingine mjini Eldoret ni hoteli Mpya ya Lincoln. Hoteli hii si nzuri kuliko Sirikwa, lakini chumba ni bei nafuu.

Kuna watu matajiri na maskini pia mjini Eldoret. Karibu sana ya Eldoret kuna mtaa mchafu wa nyumba mbovu na watu wanyonge maskini. Mtaa huu unaitwa Silas. Watu wanaokaa huko ni maskini sana na mara kwa mara watu hawa wana ukimwi. Katika utamaduni wa Kenya ukimwi una maana mbaya kwa hivyo watu wenye ukimwi hawana matumaini mengi. Lakini wamisionari na pia wafanya kazi wa Umoja wa Mataifa wanajaribu kuwasaidia watu wenye ukimwi na kumaliza ukahaba.

Kama utakuwa mgonjwa unapokaa mjini Eldoret unaweza kwenda kwa Hospitali ya Mafunzo ya Moi. Ni hospitali nzuri sana na ni mshiriki wa Hospitali ya Indiana. Pia hospitali ni mshiriki wa Chuo Kikuu cha Moi mjini Eldoret. Ilijengwa mwaka wa elfu moja mia tisa na ishirini, na ilitanuka mwaka wa elfu moja mia tisa sabini na tatu na tena mwaka wa elfu moja mia tisa themanini na sita. Ina konde kubwa lakini haitumii konde lote. Lakini kuna vitanda zaidi ya mia tatu. Sasa, hospitali hii inafanya kazi kupigana na kushinda ukimwi.

Eldoret si mji mkubwa sana hasa kufanana miji ya Marekani. Lakini watu wengi wanaenda mjini Eldoret, na mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na tisa kulikuwako watu laki moja elfu tisini na tatu mia themanini, na thelathini. Sasa Eldoret ni mji mkubwa wa tano nchini Kenya.

Eldoret ni mji mzuri sana, kama unavyoweza kuona kutoka kwa mifano iliyotolewa. Kama utakuwa na nafasi uende mjini Eldoret.

Marejeleo

http://en.wikipedia.org/wiki/Eldoret

http://www.mu.ac.ke/

http://www.mu.ac.ke/eldoret/eldphoto.html

http://www.world66.com/africa/kenya/theriftvalley/eldoret

http://www.nationmedia.com/dailynation/nmgcontententry.asp?category_id=3&newsid=92313